

UKWELI UNAPASHWA KUJUWALI.

VIRUSI VYA AINA YA DELTA: UNACHOHITAJI KUJUA

Virusi hubadilika kila wakati. Mabadiliko makubwa yanapotokea, wanasayansi huiita aina mpya. Aina zingine hazina madhara makubwa, ilhali zingine ni hatari.



Aina ya Delta inachunguzwa zaidi na wanasayansi kwa sababu ni rahisi kuambukizwa na kuenea kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine na inaweza kusababisha mtu kuugua vikali.



Watu wengi wa kila umri wanaugua kutokana na Delta, wakiwemo watu wazima, vijana na watoto.

CHANJO HUKULINDA DHIDI YA MAAMBUKIZI YA AINA YA DELTA

Njia bora ya kujilinda, kuilinda familia na jamii yako dhidi ya virusi vya aina ya Delta ni kupokea chanjo kamili. Chanjo ni:

- ✓ **SALAMA:** Chanjo imethibitishwa kuwa salama kwa mamilioni ya watu, ikiwemo kwa watu wa jamii, kabila na umri mbalimbali. Kuna uwezekano mkubwa kuwa utaugua zaidi kutokana na maambukizi ya COVID-19 au virusi vya Delta kuliko kutokana na chanjo.
- ✓ **ZENYE UFANISI** Chanjo inakuinga dhidi ya COVID-19 na virusi vya aina ya Delta. Chanjo pia inakuzuia usiugue sana na usifariki unapokuwa mgonjwa.
- ✓ **HAILIPISHWI:** Chanjo inatolewa bila malipo kwa watu wote, bila kujali hali yako ya uhamiaji au ikiwa una kitambulisho au bima ya matibabu.



Ikiwa hujapewa chanjo, kuna uwezekano mkubwa wa kuambukizwa virusi vya aina ya Delta, kuugua vibaya, na kuwaambukiza wengine.

UNAWEZA KUZUIA MSAMBAO WA AINA HATARI ZA VIRUSI KWA KUPOKEA CHANJO



Aina hatari zaidi za virusi kama vile Delta zimeibuka kwa sababu ni watu wachache pekee wamepewa chanjo. Huenda kukazuka aina zingine kama Delta katika siku zijazo. Njia bora ya kujilinda, kuilinda familia na jamii yako ni kupokea chanjo mapema iwezekanavyo. Saidia kukomesha COVID-19.




Chanjo zingine zinatolewa kupitia dozi mbili. Inachukua wiki mbili baada ya dozi yako ya mwisho ili uwe umejikinga kikamilifu.

JILINDE NA UILINDE JAMII YAKO DHIDI YA VIRUSI VYA AINA YA DELTA

Virusi vya aina ya Delta vinaenea kwa urahisi zaidi kuliko aina zingine za COVID-19. Ikiwa hujapata chanjo kamili, jilinde na uilinde jamii yako kwa:



Kuvaa maski.



Kutokaribiana na watu.



Kuepuka mahali penye watu wengi.



Kua viini kwenye sehemu zinazoguswa mara kwa mara.



Kunawa mikono mara kwa mara.

Wataalamu wengi wa afya bado wanapendekeza kuwa waliopewa chanjo wazingatie tahadhari hizi pia, hasa wakiwa mahali penye watu wengi au ikiwa wamekusanyika



UNAWEZA KUZUIA MSAMBAO WA AINA HATARI ZA VIRUSI KWA KUPOKEA CHANJO

SAIDIA KUKOMESHA COVID-19.